**Lengo>>Kuondoa migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji**

# DC Kiteto awapa somo wakulima, wafugaji kuhusu utunzaji ardhi

**Na LILIAN JOEL,** *Kiteto*

MKUU wa Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Tumaini Magesa, amewataka wafugaji na wakulima katika vijiji vya Kimbo, Allole na Napalai, vinavyounda ushirika wa "Olengapa" kutunza ardhi kwa ajili ya malisho ya mifugo, kuheshimu utaratibu wa hati miliki za kimila na usajili wa ushirika huo.

Tumaini alitoa rai hiyo jana katika Kijiji cha Engang'ongare, wakati akikabidhi hati miliki za kimila tisa na vyeti, zilizofadhiliwa na Programu ya GSI-ICCA kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na kusaidiwa na Umoja wa Ulaya (EU), kupata usajili wa usharika wao katika vijiji hivyo.

Alisema lengo la UNDP na EU kuwasaidia wafugaji hao kwa ajili ya kuendeleza nyanda za malisho, zilizopo katika mpango wa kimataifa wa kuendeleza maeneo yaliyohifadhiwa kwa kutumia taratibu za kiasili au kimila na kutekelezwa na Jumuiko la Mali Asili Tanzania (TNRF) na Muungano wa Vijiji vya Wafugaji kwa Ajili ya Kusaidiana (KINNAPA).

Magesa alisema ni vizuri kila eneo matumizi yake yawe yamepangwa na kujulikana kisheria, ili kuondoa changamoto ya migogoro ya ardhi, iliyokuwa ikijitokeza wilayani humo, miaka iliyopita.

"Tunapotunza ardhi hizi tunaondokana na migogoro isiyo ya lazima, lakini tunahifadhia vizazi vijavyo na vya sasa,"alisema.

Kwa upande wake mmoja wa wananchi hao kutoka kijiji cha Kimbo akizungumza kwa niaba ya wenzake, Rehema Barhe, alisema wao kama wanawake wa jamii ya kifugaji na wananchi wengine, wamefurahia mpango huo ambao utakuwa chachu kubwa ya kupiga hatua ya maendeleo na kumaliza changamoto ya migogoro ya ardhi iliyokuwa ikijitokeza baina ya wafugaji na wakulima.

Mkurugenzi wa Jumuiko la Mali Asili Tanzania (TNRF), Zacharia Fustin, alisema hatua ya serikali kuruhusu sera na sheria zitumike kutatua migogoro ya ardhi, pamoja na kukabidhi hati miliki za Kimila kwa jamii ya kifugaji, kutamaliza migogoro ya rasilimali ardhi kwa wakulima na wafugaji.

Mratibu wa KINNAPA, Abrahamu Akilimali alisema lengo la mpango huo kuhakikisha maeneo yaliyohifadhiwa kiasili yawe na umiliki wa kisheria ili kutunza na kulinda rasilimali ardhi na asili, pamoja na kumaliza migogoro ya ardhi.

Hati miliki za kimila tisa na vyeti vitatu vya usajili wa ushirika wa wafugaji wa kuendeleza nyanda za malisho,vilivyotolewa kwa vijiji vitatu, vimehusisha ukubwa wa eneo la ardhi kilomita za mraba 7,348.

KIKAO

Scanned with CamScanner

halmashauri hiyo, Boniface Butondo (kushoto), mjini Kishapu, mwishoni mwa wiki. (Picha na Salvatory Ntandu).

UHURU 4K15.

# *Mwanri aagiza kukamatwa kwa wafugaji wanaodaiwa kumshambulia mkulima*

**Na ALLAN KITWE,** *Sikonge*

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri ameiagiza Polisi wilayani Sikonge mkoani humo kuwakamata wafugaji waliomshambulia kwa kumkata mapanga mkulima Said Aman, mkazi wa kijiji cha Muungano, kata yaTutuo wilayani humo ambao awali walikamatwa na kuachiwa kinyemela.

Alitoa agizo hilo juzi alipokuwa katika ziara ya siku moja wilayani humo baada ya kulalamikiwa na wakazi wa kata hiyo kuwa baadhi ya wafugaji wamekuwa na tabia ya kulisha mifugo katika mashamba ya wakulima kwa makusudi na wakizuiwa wanawashambulia.

Mwanri aliagiza vyombo vya ulinzi na usalama wilayani humo kuwasaka wafugaji hao ambao awali walikamatwa, ambao wanadaiwa kuachiwa kinyemela ili wafikishwe katika vyombo vya sheria kwa tuhuma za kumkata mapanga mkulima huyo.

Pia, aliwataka wakulima hao kuwa watulivu wakati serikali ikiendelea na juhudi za kutafuta suluhu ya mgogoro huo huku akiagiza pia vyombo hivyo kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini na kukamatwa wale wote wanaosababisha migogoro hiyo.

Awali, wakulima hao waliomba serikali ya mkoa kuingilia kati vitendo hivyo kwa kuwa vimekuwa vikisababisha waishi kwa hofu kubwa huku baadhi yao wakiogopa hata kwenda katika mashamba yao.

Walidai hivi karibuni mwenzao alikatwa panga kichwani na mmoja wa wafugaji aliyemkuta akilisha mifugo kwenye shamba lake na baada ya kutoa taarifa polisi wafugaji wawili walikamatwa lakini wakaachiliwa.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Ally Mtwale, alikiri kupokea taarifa ya uwepo wa matukio ya wafugaji kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima na taarifa ya mwananchi kukatwa panga kichwani na wafugaji.

Alifafanua kuwa mkulima huyo alishambuliwa wakati akijaribu kuzuia mifugo isiendelee kuharibu mazao yake, tukio ambalo lilisababisha kupelekwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora Kitete, ambapo alilazwa na kupatiwa matibabu.

> **"Mkulima huyo alishambuliwa wakati akijaribu kuzuia mifugo isiendelee kuharibu mazao yake, tukio ambalo lilisababisha kupelekwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora Kitete, ambapo alilazwa na kupatiwa matibabu.**
>
> Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Muungano, Ally Mtwale

Kamishna Msaidizi Kamanda Sadi aliwataka wananchi

*

# UFUGAJI

*

UHURU UK 19.



**WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene (kushoto), akiangalia ng'ombe wanaofugwa na Gereza la Mifugo Ubena, Bwawani, mkoani Pwani, jana. Wapili kulia ni Mkuu wa Gereza hilo, Daimu Mmolosha.** (Picha na Wizara ya Mambo ya Ndani).

Scanned with CamScanner